# NISHATI

HABARI ZA NISHATI

# News Bulletin

www.nishati.go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati

**Toleo Namba 32** | **Novemba 1 - 30, 2021**


# MAKAMU WA RAIS APONGEZA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE

## • Ataka umakini



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Philip Isdor Mpango (kulia) akizungumza na Waziri wa Nishati, January Makamba (katikati) na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato wakati alipofika katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ili kukagua utekelezaji wake.*


**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au

**Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma**

# Makamu wa Rais apongeza utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Philip Isdor Mpango amekagua utekelezaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) na kupongeza hatua za ujenzi zilizofikiwa.

Alitoa pongezi hizo tarehe 12 Oktoba, 2021 wakati akitembelea maeneo mbalimbali ya mradi huo unaotekelezwa katika mkoa wa Pwani na Morogoro akiwa ameambatana na viongozi mbalimbali wa Wizara ya Nishati na Mikoa ya Pwani na Morogoro wakiongozwa na Waziri wa Nishati, January Makamba.

Maeneo aliyotembelea ni pamoja na ujenzi waTuta kuu la Bwawa, Njia za kupeleka maji kwenye mitambo itakayofua umeme, Jengo la mitambo pamoja na ujenzi wa kituo cha kupokea na kusafirisha umeme.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Philip Isdor Mpango (kushoto) akisalimiana na viongozi mbalimbali wa Wizara ya Nishati, Mkoa wa Pwani na Morogoro mara alipofika katika eneo kunapotekelezwa mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP). Katikati ni Mke wa Makamu wa Rais, Mbonimpaye Mpango.*

"Mheshimiwa Waziri wa Nishati pamoja na TANESCO nawapongeza kwa kuendelea kusimamia ujenzi wa mradi huu, mnafanya kazi nzuri sana, Serikali inawapongeza na jicho la Serikali liko hapa kwani tuliwaahidi Watanzania kwamba tutaujenga mradi huu ili tupate umeme wa kutosha utakaojenga uchumi wa viwanda," alisema Makamu wa Rais

Aliwataka viongozi hao kuendelea kuchapa kazi, kutanguliza uzalendo na kuwa makini ili kuhakikisha kwamba mradi huo unakamilika kwa viwango vinavyotakiwa.

Akiwa kwenye eneo unakoendelea ujenzi wa Tuta kuu la bwawa, Makamu wa Rais aliwaelekeza wasimamizi wa mradi huo kuhakikisha kuwa kila kitu kinatekelezwa kwa umakini mkubwa ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea endapo mradi huo utaanza kufanya kazi huku ukiwa na mapungufu.

"Ninyi kama wasimamizi wa mradi, mhakikishe kwamba kama kuna hitilafu inaonekana ifuatiliwe kwa ukamilifu, ikitokea tatizo lolote la kiufundi na hili bwawa likapasuka hapo baadaye madhara huko mbele yatakuwa makubwa, hatutaki kuingiza nchi yetu



*Waziri wa Nishati, January Makamba (katikati) akizungumza jambo na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Philip Isdor Mpango (kushoto) wakati alipotembelea mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP). Wa Pili kushoto ni Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato na kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigellah.*



*Kazi za ujenzi zikiendelea katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere utakaozalisha umeme wa kiasi cha megawati 2115.*

# Makamu wa Rais apongeza utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Philip Isdor Mpango (kushoto) akizungumza na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (wa Tatu kutoka kulia), Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Felchesmi Mramba (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande ( wa kwanza kulia) mara alipofika katika eneo la mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ili kukagua utekelezaji wake.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Philip Isdor Mpango (wa Pili kushoto) akizungumza jambo wakati alipofanya ziara katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ili kuona utekelezaji wake. Wa kwanza kushoto ni Mke wa Makamu wa Rais, Mbonimpaye Mpango, Wa Nne kutoka kushoto ni Waziri wa Nishati, January Makamba na Wa Tatu kutoka kushoto ni Mhandisi Mkazi wa Mradi wa Julius Nyerere, John Mageni.*

kwenye historia mbaya," alisisitiza Makamu wa Rais

Aliongeza kuwa, taratibu zote za kitalaam zifuatiliwe na vigezo vizingatiwe kwa asilimia 100 na hata kama kuna hitilafu ndogo ifuatiliwe chanzo chake kwa maslahi mapana ya nchi.

Alitaja gharama za utekelezaji wa mradi huo ni shilingi Trilioni 6.5 na kuwaasa watanzania kuendelea kulipa kodi ambayo ndiyo inayotekeleza miradi mikubwa kama huo wa bwawa la Julius Nyerere.

Kwa upande wa mazingira aliagiza kuwa kuwe na usimamizi mkubwa wa masuala yote yatakayoathiri ujazaji maji katika bwawa hilo ili ndoto ya kuzalisha umeme katika bwawa hilo itimie.

"Siyo tujenge tu bwawa zuri lakini tukaja hapo baadae tukaliharibu, hivyo nawaombeni wakuu wa Mikoa, Wabunge na Wakuu wa Wilaya kuendelea kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuhakikisha kwamba mazingira ya maeneo yanayohusu mradi huo yanabaki salama na safi ili bwawa litupatie kile tunachokitaka kama vile umeme, uvuvi, umwagiliaji na utalii," alisema Makamu wa Rais.

Awali, Waziri wa Nishati, January Makamba, alimshukuru Makamu wa Rais kuwa, kwa kutembelea mradi huo na kuelekeza kuwa hiyo inaonesha jinsi Serikali ya Awamu ya Sita inavyotoa uzito na kuupa umuhimu mradi huo wa JNHPP.

Alisema kuwa, Wizara ya Nishati pamoja na TANESCO wanafahamu dhamana kubwa waliyokabidhiwa na nchi katika kusimamia mradi huo ambao una maana kubwa kwa Taifa na ni ishara na kielelezo cha maono makubwa ambayo viongozi wamekuwa nayo, kielelezo cha Taifa linalotaka kupiga hatua mbele na pia ni kielelezo cha kusukuma maendeleo na kuwajali wananchi.

Alieleza kuwa, Wizara ya Nishati pamoja TANESCO wanachukulia dhamana hiyo kwa uzito mkubwa na heshima kubwa hivyo ahadi wanayoitoa ni kutimiza wajibu kwa uadilifu na weledi ili kutowaangusha Viongozi wa Nchi na watanzania kwa ujumla.

Viongozi wa Wizara ya Nishati walioambatana na Makamu wa Rais katika ziara hiyo ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Felchesmi Mramba na Wakuu wa Idara na Vitengo mbalimbali.

# MAKAMU WA RAIS ATOA MAELEKEZO MAHSUSI KUBORESHA UTEKELEZAJI WA MRADI WA JULIUS NYERERE (JNHPP)

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Philip Isdor Mpango ametoa maelekezo mbalimbali kwa Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) yatakayoboresha utekelezaji Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ili uweze kukamilika kwa wakati uliopangwa.

Maelekezo hayo aliyatoa tarehe 13 Oktoba, 2021 wakati wa kikao cha majumuisho ya ziara yake ya siku mbili ya kutembelea mradi huo wa JNHPP kilichofanyika katika eneo la Mradi na kuhudhuriwa na Viongozi mbalimbali wakiongozwa na Waziri wa Nishati, January Makamba.

Baadhi ya maelekezo yake ni kuwa, Katibu Mkuu Kiongozi ateue timu ya wataalam kutoka Wizara mbalimbali, baadhi ya Taasisi za Serikali na vyombo vya Ulinzi na Usalama itakayochambua changamoto mbalimbali zinazohusu mradi huo na kupendekeza utatuzi wake.

“Timu ya hiyo ya Serikali ichambue changamoto hizo na kupendekeza ushauri wake, ikiwemo suala la ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka eneo la mradi hadi mji wa Chalinze na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme,” alibainisha Makamu wa Rais

Alielekeza kuwa, TANESCO ijenge njia hiyo ya kusafirisha umeme kutoka eneo hilo la mradi kwenda Chalinze na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Chalinze ili kuwezesha majaribio ya kuzalisha umeme mara mradi utakapokamilika.

Maelekezo mengine ni pamoja na TANESCO kuwa na wataalam wa kutosha katika nyanja mbalimbali ikiwemo Wahandisi, Wanasheria, Wasanifu na Wahandisi wa mabwawa ya kufua umeme watakaowezesha Shirika hilo kufanya kazi kwa ufanisi ikiwemo ya usimamizi wa mradi huo.

“Angalieni uwezekano wa kuongeza wataalam sehemu zenye mapungufu, mkandarasi aongeze vitendea kazi vinavyohitajika, na pia muda wa kufanya kazi uangaliwe ili mradi huu ufanikiwe,” alisisitiza Makamu wa Rais

Pia, alimuelekeza Waziri wa Nishati kufuatilia masuala yanayohusu fedha zinazotengwa kwa ajili ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) ili yafanyike kwa ufanisi.

Kwa upande mwingine, alielekeza Wizara ya Nishati, TANESCO na mkandarasi wa mradi kukutana ili kujadili namna ya kufidia muda uliopotea kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo UVIKO 19 katika utekelezaji wa mradi huo.

Aidha aliagiza kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu isaidie kuharakishwa kwa upatikanaji wa vibali vya



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Philip Isdor Mpango (katikati) akizungumza wakati wa kikao cha majumuisho mara baada ya kumaliza ziara yake katika mradi wa Umeme wa Julius Nyerere. Kushoto ni Waziri wa Nishati, January Makamba na kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.*



*Waziri wa Nishati, January Makamba (kushoto) akizungumza wakati wa kikao cha majumuisho mara baada ya kumalizika kwa ziara ya Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Tanzania, Mhe.Philip Isdor Mpango (katikati) katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere. Kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.*

# MAKAMU WA RAIS ATOA MAELEKEZO MAHSUSI KUBORESHA UTEKELEZAJI WA MRADI WA JULIUS NYERERE (JNHPP)




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Philip Isdor Mpango (wa Tano kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na Wakuu wa mikoa ya Morogoro na Pwani mara baada ya kumaliza kikao cha majumuisho kilichofanyika katika mradi wa Umeme wa Julius Nyerere. Wa Tatu kulia ni Mke wa Makamu wa Rais, Mbonimpaye Mpango, Wa Nne kushoto ni Waziri wa Nishati, January Makamba, Wa Pili kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato na wa kwanza kulia ni Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali.*

wataalam kutoka nje ya nchi wanaoingia nchini kufanya kazi kwenye mradi huo.

Kwa upande wake, Waziri wa Nishati, January Makamba alimshukuru Makamu wa Rais kwa kutembelea mradi wa JNHPP na kutoa maelekezo hayo na kuahidi kuanza kuyafanyia kazi mara moja.

Viongozi mbalimbali waliohudhuria kikao hicho cha majumuisho ni pamoja na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigellah, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande na watendaji wengine kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO.



*Watendaji mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati, TANESCO, Mkoa wa Morogoro na Pwani, wakimsikiliza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Philip Isdor Mpango (hayupo pichani) wakati wa kikao cha majumuisho mara baada ya kumaliza ziara yake katika mradi wa Umeme wa Julius Nyerere.*




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Philip Isdor Mpango (wa Tano kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali kutoka TANESCO na Wakuu wa mikoa ya Morogoro na Pwani mara baada ya kumaliza kikao cha majumuisho kilichofanyika katika mradi wa Umeme wa Julius Nyerere. Wa Tatu kulia ni Mke wa Makamu wa Rais, Mbonimpaye Mpango, Wa Nne kushoto ni Waziri wa Nishati, January Makamba, Wa Pili kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato na wa kwanza kulia ni Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali.*




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Philip Isdor Mpango (wa Tano kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali kutoka, Wizara ya Nishati, TANESCO na Wakuu wa mikoa ya Morogoro na Pwani mara baada ya kumaliza kikao cha majumuisho kilichofanyika katika mradi wa Umeme wa Julius Nyerere. Wa Tatu kulia ni Mke wa Makamu wa Rais, Mbonimpaye Mpango, Wa Nne kushoto ni Waziri wa Nishati, January Makamba, Wa Pili kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, wa kwanza kulia ni Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, Wa Nne kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, Wa Tatu kushoto Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigellah na Wa Pili kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande.*

# Waziri Makamba akutana na Waziri wa Nishati Saudi; awasilisha ujumbe wa Rais Samia

**Riyadh, Saudi Arabia**

Waziri wa Nishati, January Makamba amekutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia, Abdulaziz bin Salman Al Saud ikiwa ni siku ya pili ya ziara ya kikazi nchini humo.

Katika kikao hicho, Waziri Makamba alijadiliana masuala mbalimbali yahusuyo nishati na Waziri mwenzake na pia aliwasilisha ujumbe maalumu kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa Serikali ya Saudi Arabia.



*Waziri wa Nishati, January Makamba akiongozana na mwenyeji wake ambaye ni Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia, Abdulaziz bin Salman Al Saud mara baada ya kumaliza kikao chao kilicholenga kudumisha uhusiano katika sekta ya nishati na kuwasilisha ujumbe wa Rais Samia kwa Serikali ya Saudi Arabia.*

Akizungumza baada ya kikao hicho, Waziri Makamba alisema "tumekuja nchini Saudi Arabia tukiwa na ujumbe maalumu kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ninayo furaha kusema kuwa ujumbe huo umefika kama ilivyokusudiwa". Aidha, Waziri Makamba aliongeza kuwa Tanzania na Saudi Arabia zina mahusiano mazuri ya muda mrefu na sasa nchi hizi mbili zinakusudia kuendeleza mahusiano kwa kuongeza ushirikiano katika sekta ya nishati.

"Katika kuthibitisha hilo siku za hivi karibuni Waziri wa Mambo ya



*Waziri wa Nishati, January Makamba akizungumza na mwenyeji wake, Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia Abdulaziz bin Salman Al Saud.*



*Waziri wa Nishati, January Makamba akiagana na mwenyeji wake, Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia, Abdulaziz bin Salman Al Saud mara baada ya kumaliza mazungumzo yao. Wengine pichani ni Balozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia, Balozi Ali J. Mwadini (nyuma ya Waziri Makamba), Kamishna wa Petroli na Gesi, Ndg. Michael Mjinja (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio (kushoto)*

# Waziri Makamba akutana na Waziri wa Nishati Saudi; awasilisha ujumbe wa Rais Samia

Nje wa Saudi Arabia alitembelea Tanzania na pia Mfalme wa Saudi, Mfalme Salman bin Abdulaziz Al Saud amemualika Rais wetu, Mhe. Samia Suluhu Hassan kuzuru Saudi Arabia" alieleza zaidi Waziri Makamba.


Waziri Makamba, katika ziara hiyo ameambatana na Kamishna wa Petroli na Gesi, Ndg. Michael Mjinja na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio.

Ziara hiyo pia imelenga kuanzisha uhusiano wa kibiashara, kubadilishana ujuzi na teknolojia katika sekta ya mafuta na gesi. Ikumbukwe kuwa Saudi Arabia ni mzalishaji mkubwa wa mafuta duniani na hivyo mahusiano na Tanzania yanaweza kufungua fursa mbalimbali katika eneo hilo.



*Waziri wa Nishati, January Makamba akiteta jambo na mwenyeji wake ambaye ni Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia, Abdulaziz bin Salman Al Saud. Wengine pichani ni Balozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia, Balozi Ali J. Mwadini (wa pili kushoto) na Katibu wa Waziri Makamba, Ndg. Dunford Mpelumbe (wa kwanza kushoto)*

# Waziri Makamba awasilisha ujumbe wa Rais Samia kwa Serikali ya Algeria



*Waziri wa Nishati, January Makamba akiwa katika mazungumzo na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, Aymen Benabderrahmane mara baada ya kukabidhi ujumbe maalumu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa Serikali ya Algeria. Katika kikao hicho Waziri makamba aliambatana na Balozi wa Tanzania nchini Algeria, Balozi Meja Jenerali Jacob Gideon Kingu, Kamishna wa Petroli na Gesi kutoka Wizara ya Nishati, Michael Mjinja na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio.*

**Algiers. Algeria,**

Ziara ya Waziri wa Nishati, January Makamba nchini Algeria imezidi kufungua fursa za ushirikiano baina ya Tanzania na Algeria ikiwa ni nchi marafiki tangu enzi za ukombozi wa Afrika.

Waziri Makamba ametembelea Algeria kwa lengo la kukuza uhusiano wa kisekta na pia kuwasilisha ujumbe maalumu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria.

Ujumbe huo maalumu kutoka Serikali ya Tanzania kwa Serikali ya Algeria ulipokelewa na Waziri Mkuu wa Algeria, Mhe. Aymen Benabderrahmane kwa niaba ya Rais wa Algeria, Mhe. Abdelmadjid Tebboune.

Akiongea baada ya kupokea ujumbe huo, Mhe. Benabderrahmane alisema "Tanzania na Algeria ni marafiki wa kihistoria na ni wakati muafaka kwa nchi hizi mbili kuboresha zaidi mahusiano na namna moja wapo wa kufanya hivyo ni kushirikiana kiuchumi kwa manufaa ya wananchi wa nchi zote mbili".

Aidha Waziri Mkuu huyo alieleza kuwa kuna maeneo mengi ya kiuchumi ambayo Tanzania na Algeria wanaweza kushirikiana na eneo mojawapo ni sekta ya nishati ambayo Algeria ina uzoefu wa zaidi ya miaka 50 huku ikiwa na ugunduzi mkubwa wa mafuta na gesi asilia.

Aidha Waziri Makamba alieleza nia ya Serikali ya Tanzania kuanzisha uhusiano na Algeria katika eneo la nishati ambapo tayari nchi hizi mbili zilishaanzisha majadiliano na hata kuandaa rasimu ya hati ya makubaliano (Memorandum of Understanding-MoU) katika maeneo ya gesi asilia na umeme.

"Tayari kuna kazi kubwa ilikwishafanyika huko nyuma na ziara hii imelenga kuhakikisha kazi hiyo kubwa inakamilika ili kuona urafiki wetu unaimarika zaidi kwa kushirikiana katika kukuza uchumi" alisema Waziri Makamba

Mara baada ya kuwasilisha ujumbe huo, Waziri Makamba alipata nafasi ya kutembelea kampuni za Sonelgaz na Sonatrach ambazo ni kampuni za Serikali zinazojihusisha na mnyororo mzima wa thamani wa sekta ya nishati (mafuta, gesi na umeme).

Kwa upande wa Sonelgaz, Waziri Makamba alitembelea kituo cha kuzalisha umeme ambapo aliweza kujionea matumizi makubwa ya teknolojia katika kuendesha na kusimamia gridi ya taifa



*Waziri wa Nishati, January Makamba akiwa katika mazungumzo na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, Aymen Benabderrahmane mara baada ya kukabidhi ujumbe maalumu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwa Serikali ya Algeria.*

# Waziri Makamba awasilisha ujumbe wa Rais Samia kwa Serikali ya Algeria



*Waziri wa Nishati, January Makamba akizungumza jambo na Mkurugenzi Mkuu wa Sonelgaz, Chahar Boulakhras wakati alipofanya ziara ya kutembelea kituo cha kuzalisha umeme Jijini Algiers kinachoedeshwa na Sonelgaz. Wengine pichani kutoka kushoto ni Mwambata wa Jeshi katika Ubalozi wa Tanzania nchini Algeria, Brigedia Jenerali Adolf Peter Mutta, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio na Kamishna wa Petroli na Gesi kutoka Wizara ya Nishati, Ndg. Michael Mjinja.*

ya umeme.

"Nimeweza kuona namna wenzetu wanatumia teknolojia katika kusimamia gridi na hii ni moja ya eneo ambalo tunaweza kushirikiana kwa kubadilishana ujuzi na uzoefu", alisema Waziri Makamba.

Pamoja na kuwa Algeria ni nchi kubwa kuliko zote Afrika kwa eneo lakini wameweza kusambaza umeme kwa zaidi ya asilimia 90 ya watu wake na pia kujenga mtandao wa kusambaza gesi asilia wa kilometa 22,000.

Akitoa maelezo wakati wa ziara hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa Sonelgaz, Chahar Boulakhras alimueleza Waziri Makamba kuwa Sonelgaz iko tayari kuwekeza Tanzania na itasubiri mualiko rasmi ili kutuma timu ya wataalam kuendeleza mazungumzo ambayo yalikwishaanza hapo awali.

Kwa upande wa Sonatrach, Waziri Makamba alitembelea moja ya kiwanda cha kusafisha mafuta kilichopo Algiers ambapo alijionea namna shughuli za usafishaji mafuta ghafi zinavyofanyika na bidhaa mbalimbali zinazozalishwa kiwandani hapo ikiwemo dizeli, petroli, JET A1 na gesi ya mitungi (LPG).

Akizungumza baada ya kutembelea kiwanda hicho, Waziri Makamba alisema "Tumejionea namna hawa wenzetu walivyopiga hatua katika eneo hili na ninaamini Tanzania tunaweza kujifunza na kujenga mahusiano zaidi ya kibiashara na Algeria kwa maslahi mapana ya nchi zetu".

Akizungumza baada ya kumaliza ziara yake nchini Algeria, Waziri Makamba alisema "Tunatarajia kuwaalika wataalamu kutoka Algeria kuja nchini Tanzania kwa lengo la kukamilisha rasimu za hati ya makubaliano ambazo zilishafanyiwa kazi huko nyuma ili kuweza kuanza ushirikiano wetu mara moja bila kuchelewa".

Katika ziara hiyo, Waziri Makamba aliambatana na Kamishna wa Petroli na Gesi kutoka Wizara ya Nishati, Michael Mjinja na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio wakisindikizwa na Balozi wa Tanzania nchini Algeria, Meja Jenerali Jacob Gideon Kingu, Mwambata wa Jeshi, Brigedia Jenerali Adolf Peter Mutta, Mwambata wa Siasa na Utamaduni Ubalozi wa Tanzania nchini Algeria, Suleiman Rashid na maafisa wengine kutoka Ubalozi wa Tanzania nchini Algeria.



*Waziri wa Nishati, January Makamba akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Sonelgaz, Chahar Boulakhras (wa nne kutoka kulia) pamoja na Balozi wa Tanzania nchini Algeria, Meja Jenerali Jacob Gideon Kingu (wa tatu kutoka kulia), Kamishna wa Petroli na Gesi, Michael Mjinja (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio ( wa pili kushoto). Wengine pichani ni maafisa waandamizi kutoka Sonelgaz.*

# WATANZANIA KUNUFAIKA NA MIRADI YA NISHATI

**Hafsa Omar-Dodoma**

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amesema Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa miradi yote inayotekelezwa na Wizara ya Nishati inawanufaisha watanzania wote kwa ujumla.

Aliyasema hayo, Oktoba 25,2021,kwenye Warsha juu ya Sekta ya Uziduaji kwenye Madini, Mafuta na Gesi iliyoandaliwa na HakiRasilimali katika wiki ya Azaki 2021, jijini Dodoma.

Wakili Byabato, aliitaja baadhi ya miradi hiyo ni Mradi wa Kuchakata na kusindika gesi Asilia (LNG) na mradi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki( EACOP) ambapo ameeleza kuwa miradi hiyo ipo katika hatua za utekelezwaji wake.




*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza kwenye Warsha juu ya Sekta ya Uziduaji kwenye Madini, Mafuta na Gesi iliyoandaliwa na HakiRasilimali katika wiki ya Azaki 2021, iliyofanyika jijini Dodoma. Oktoba 25,2021.*

Alisema, Wizara imelielekeza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ipite katika mikoa yote Nane ambayo bomba la mafuta linapita na kubaini fursa mbalimbali ambazo zinapatikana katika mikoa husika ili watanzania wazijue na waweze kunufaika nazo.

" Serikali ya Awamu ya Sita imetoa maelekezo mahsusi kabisa kuwa kila Mtanzania anufaike na ashiriki katika miradi hii na sisi Wizara ya Nishati tumeshaweka utaratibu kwa upande wa bomba la mafuta TPDC itaenda kwenye Mikoa yote kuangalia kwa namna gani fursa zilizopo katika maeneo hayo zitawanufaisha Watanzania," alisema

Kwa upande wa mradi wa Gesi, Wakili




*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kwanza- kulia) akimsikiliza Waziri wa Madini, Doto Biteko (Pili-kulia) wakati akizungumza kwenye Warsha juu ya Sekta ya Uziduaji kwenye Madini, Mafuta na Gesi iliyoandaliwa na HakiRasilimali katika wiki ya Azaki 2021, iliyofanyika jijini Dodoma, Oktoba 25, 2021. Wa Tatu kutoka kulia ni Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe.*

# WATANZANIA KUNUFAIKA NA MIRADI YA NISHATI

Byabato alieleza kuwa Wizara ya Nishati inatambua kuwa jukumu la kuhakikisha mradi wa Gesi wa LNG unaanza mara moja na kwa kuzingatia hilo Majadiliano baina ya timu ya majadiliano ya Serikali na wawekezaji ya mradi huo itaanza kazi rasmi Novemba 8, 2021.

Aidha, alieleza kuwa mradi huo utakapokamilika utakuwa na manufaa mengi kwa Taifa kwa ujumla wake, ambapo gesi nyingi itapatikana ambayo itatosheleza kwa matumizi ya ndani na pia itaweza kuuzwa nje ya nchi ambapo nchi itaweza kujiongezea pato la Taifa.



*Wadau mbalimbali wakisikiliza mada mbalimbali ambazo zilikuwa zikitolewa kwenye Warsha juu ya Sekta ya Uziduaji kwenye Madini, Mafuta na Gesi iliyoandaliwa na HakiRasilimali katika wiki ya Azaki 2021, iliyofanyika jijini Dodoma. Oktoba 25,2021.*




*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akisikiliza mada mbalimbali zilizokuwa zikitolewa kwenye Warsha juu ya Sekta ya Uziduaji kwenye Madini, Mafuta na Gesi iliyoandaliwa na HakiRasilimali katika wiki ya Azaki 2021, iliyofanyika jijini Dodoma. Oktoba 25,2021.*

Sambamba na hilo, alisema kuwa Watanzania wanaendelea kunufaika na matumzi ya Gesi majumbani na kwenye viwanda ambapo alieleza kuwa wananchi wengi wa Mkoa wa Mtwara walinufaika na gesi hiyo.

Alieleza kuwa, huo ni mkakati endelevu wa kusambaza gesi majumbani na Serikali itahakikisha kwamba inafika kwa kila Mtanzania.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisitiza kuwa miradi hiyo ambayo inatekelezwa na Wizara ya Nishati ishirikishe watanzania walio wengi na amewaasa watanzania kuendelea kuzalisha bidhaa ambazo zitaweza kununuliwa katika miradi hiyo.

# Tanzania, Rwanda na Burundi waridhishwa na kasi ya ujezi wa mradi wa RUSUMO




*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kulia), Waziri wa Miundombinu Rwanda, Balozi Claver Gatete(katikati) ambaye ndiye alikuwa Mwenyekiti wa Mkutano wa 13 wa Mawaziri wa kujadili Mradi wa RUSUMO uliofanyika wilayani Ngara mkoani Kagera, Oktoba 9, 2021, na Waziri wa Mafuta, Nishati na Madini wa Burundi, Mhandisi Ibrahim Uwizeye(kushoto)wakisikiliza maswali kutoka waandishi wa habari (hawapo pichani)mara baada ya kumalizika kikao hicho.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato( wa nne kushoto) pamoja na Wajumbe wa Mkutano wa 13 wa Waziri wa Rwanda, Burundi na Bodi ya Mradi wa RUSUMO wa kujadili maendeleo ujenzi wa mradi huo, uliofanyika wilayani Ngara mkoani Kagera, Oktoba 9, 2021,wakipata maelezo ya maendeleo ya jenzi wa mradi huo walipofanya ziara ya kukagua mradi huo wakati wa mkutano.*

**Na Zuena Msuya, Kagera**

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amesema kuwa Mawaziri wa Nishati wa Rwanda, Burundi na wenyeji Tanzania wameridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi wa kufua umeme kwa kutumia maporomoko ya maji wa RUSUMO licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali.

Wakili Byabato alisema hayo wakati akimuwakilisha Waziri wa Nishati, January Makamba, mara baada ya kumalizika kwa Mkutano wa 13 wa Mawaziri hao wenye lengo la kujadili maendeleo ya ujenzi wa mradi wa RUSUMO uliofanyika wilayani Ngara mkoani Kagera, Oktoba 9, 2021.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Waziri wa Miundombinu Rwanda, Balozi Claver Gatete ambaye ndiye alikuwa Mwenyekiti wa kikao hicho, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato na Waziri wa Mafuta, Nishati na Madini wa Burundi, Mhandisi Ibrahim Uwizeye pamoja na Wajumbe wa Bodi wa Mradi huo.

Mradi huo utakuwa na uwezo wa kuzalisha Megawati 80, ambazo zitagawanywa katika nchi hizo tatu wanufaika ambapo kila moja itapata Megawati 26.6 kwa ajili



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato( wa nne katikati) pamoja na Wajumbe wa Mkutano wa 13 wa Waziri wa Rwanda, Burundi na Bodi ya Mradi wa RUSUMO wa kujadili maendeleo ujenzi wa mradi huo, uliofanyika wilayani Ngara mkoani Kagera, Oktoba 9, 2021, wakikagua maendeleo ya jenzi wa mradi wa huo.*

# Tanzania, Rwanda na Burundi waridhishwa na kasi ya ujezi wa mradi wa RUSUMO

ya matumizi ya nchi yake.

Alisema kuwa mpaka sasa ujenzi huo umefikia asilimia 82 ya utekelezaji wake na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba mwaka huu ambapo tayari mkandarasi amekwisha lipwa zaidi ya asilimia 100% ya kazi aliyokwisha fanya huku kazi ya ujenzi ikiendelea vizuri.

"Tumejadili kwa pamoja maendeleo ya ujenzi wa mradi huu wa Rusumo, tumeridhishwa na kasi ya ujenzi unavyoendelea, pia fedha za kuhakikisha mradi huu unakamilika kama ulivyopangwa zipo tayari. Hata hivyo alisema kuwa changamoto ya kuwepo kwa Virusi vya Corona Duniani kumesababisha baadhi ya vifaa vinavyotumika katika ujenzi wa mradi huo kuchelewa kufika kwa wakati kwa kuwa vingi vinatoka nje nchi.

Aliweka wazi kuwa mradi huo umegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni Eneo la Bwawa, Njia ya kuchepusha maji kwenda katika mitambo kuzalisha umeme ambayo ipo upande wa Tanzania, na nyingine ni Kituo cha Kupokea na Kusambaza umeme ambacho kiko upande wa Rwanda.

Alifafanua mradi huo awali ulikuwa ni kwa ajili ya kuzalisha na kusambaza umeme tu kwa nchi husika, lakini kwa sasa kituo hicho kimeongezewa uwezo wa kupokea umeme kutoka sehemu nyingine na kuusambaza,ambapo kitakuwa na uwezo wa kupokea hata umeme utakaozalishwa katika Mradi wa Julius Nyerere na kusambaza katika nchi za Rwanda, Burundi nk.

Utekelezaji wa hatua ya ujenzi wa kituo hicho cha kupokea na kusambaza umeme ambacho kipo upande wa Rwanda umekamilika kwa asilimia kubwa.

Sambamba na hilo alisema kuwa kwa nchi zote zitakaotumia umeme utakaozalishwa katika mradi wa RUSUMO ambazo ni Tanzania, Rwanda na Burundi zinaendelea na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kutoka katika mradi huo hadi katika maeneo husika.

Mradi wa RUSUMO unatekelezwa kwa gharama za Dolla za Kimarekani Milioni 340 ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia kwa ushirikiano wa nchi tatu wanufaika ambapo kila moja italipa Dolla Milioni 113.



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (wa pili kulia) akipata maelezo ya moja ya mitambo itakayotumika katika Mradi wa RUSUMO, walipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo, wakati wa Mkutano wa 13 wa Waziri wa Rwanda, Burundi na Bodi ya Mradi wa RUSUMO wa kujadili maendeleo ujenzi wa mradi huo, uliofanyika wilayani Ngara mkoani Kagera, Oktoba 9, 2021.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato( wa pili kushoto) akijadilina jambo na Wajumbe wa Mkutano wa 13 wa Waziri wa Rwanda, Burundi na Bodi ya Mradi wa RUSUMO wa kujadili maendeleo ujenzi wa mradi huo, uliofanyika wilayani Ngara mkoani Kagera, Oktoba 9, 2021, wakati wakikagua maendeleo ya jenzi wa mradi wa huo.*

# KATIBU MKUU NISHATI ASEMA MICHEZO ITUMIKE KUBORESHA AFYA NA UFANISI KAZINI

**Na Zuena Msuya**
**DODOMA**

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja ameiasa Timu ya Wanamichezo wa Wizara ya Nishati inayoshiriki Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), kutumia Michezo hiyo kama sehemu ya kuboresha Afya na ufanisi sehemu za kazi.

Mhandisi Masanja alisema hayo mkoani Dodoma wakati akitoa



*Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja( wa tano kushoto) akikabidhi mpira kwa Mwenyekiti wa Michezo wa Wizara ya Nishati, Germanus Haule( wa nne kushoto), mara baada ya kutoa nasaha kwa wanamichezo hao, Oktoba 18,2021 jijini Dodoma, wa tano kulia ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu wa Wizara hiyo, Ziana Mlawa.*



*Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu wa Wizara ya Nishati Ziana Mlawa (katikati) akizungumza na wanamichezo wa wizara hiyo (hawapo pichani) walipokuwa wakipatiwa nasaha kabla ya kwenda kushiriki Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), mkoani Morogoro Oktoba 18, 2021.*

# KATIBU MKUU NISHATI ASEMA MICHEZO ITUMIKE KUBORESHA AFYA NA UFANISI KAZINI



*Mwenyekiti wa Michezo wa Wizara ya Nishati, Germanus Haule (aliyesimama) akieleza jambo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu wa Wizara ya Nishati Ziana Mlawa (mwenye kilemba) kabla ya kupewa nasaha za kwenda kushiriki Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI),mkoani Morogoro Oktoba 18,2021.*

nasaha kwa wachezaji hao wanaokwenda kushiriki SHIMIWI mkoani Morogoro kuanzia Oktoba 20 hadi Novemba 2, 2021.

Aidha aliwataka wanamichezo hao kuheshimu Michezo hiyo na kuzingatia dhana nzima ya kuanzishwa kwake.

Vilevile aliwasihi wanamichezo hao kucheza kwa nidhamu pamoja na kuwa na mbinu za ziada ili kupata ushindi wa kishindo.

Sambamba na hilo aliwaeleza kuwa wanapokuwa kambini wanapaswa kuishi kwa nidhamu kwa mujibu wa Sheria za Utumishi wa Umma.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu wa wizara hiyo Ziana Mlawa aliwaeleza wanamichezo hao kuwa wanapokuwa kambini ni sawa na wanapokuwa maeneo yao ya kazi hivyo wafuate na kuzingatia taratibu zote za kiutumishi.

Mlawa alisema kuwa wanamichezo hao wakawe mfano bora kiutendaji kwa kushiriki mazoezi ya aina yote na yale yote wanayopaswa kufanya wanapokuwa katika michezo hiyo.

Vilevile aliwasihi kuendeleza umoja, ushirikiano kwa wanamichezo wote watakaokuwa pamoja kama wanavyoshirikiana na watumishi wengine katika Wizara ya Nishati.

Takribani wanamichezo 30 kutoka Vitengo na Idara za wizara hiyo watashiriki michezo ya Mpira wa Pete, Miguu, kuvuta kamba, kuendesha Baiskeli, mbio za Magunia nk.

Michezo ya SHIMIWI inaratajiwa kufunguliwa Oktoba 20, 2021 na kufikia kilele chake Novemba 2, 2021 mkoani Morogoro.

# WAZIRI MAKAMBA AKUTANA NA MABALOZI WA NCHI ZA KIARABU



*Waziri wa Nishati, January Makamba akizungumza na Balozi wa Saudi Arabia nchini Tanzania, Abdulaziz Hamad Alasim, Oktoba 18, 2021 katika ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dar es Salaam. Pamoja nao ni Kamishna wa Petroli na Gesi Michael Mjinja (kulia) na Sabra Omar (kushoto) aliyeambatana na Balozi.*

Waziri wa Nishati, January Makamba, Oktoba 18, 2021 kwa nyakati tofauti alikutana na kufanya mazungumzo na mabalozi wa mataifa ya Saudi Arabia, Qatar, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Algeria nchini Tanzania, kwenye ofisi ndogo za Wizara ya Nishati jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Waziri Makamba, mazungumzo hayo yalilenga kuimarisha uhusiano wa kisekta baina ya Tanzania na nchi hizo, ili kuiongezea tija sekta ya nishati kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji.

"Rais wetu Mh. Samia Suluhu Hassan yuko mstari wa mbele katika kuhakikisha sekta ya nishati inaimarika na kulinufaisha taifa kiuchumi, hususani katika kuvutia wawekezaji na kutumia vyema rasilimali za mafuta na gesi asilia," alieleza Waziri Makamba.



*Waziri wa Nishati, January Makamba akizungumza na Balozi wa Qatar nchini Tanzania Hussain Ahmad Al Homaid, Oktoba 18, 2021 katika ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dar es Salaam. Pamoja nao ni Mkalimani Fawaz Ibrahim Argof aliyeambatana na Balozi.*

# WAZIRI MAKAMBA AKUTANA NA MABALOZI WA NCHI ZA KIARABU



*Baadhi ya viongozi walioshiriki kwenye mazungumzo baina ya Waziri wa Nishati, January Makamba na mabalozi wa nchi za Saudi Arabia, Qatar za Falme za Kiarabu (UAE) wakifuatilia mazungumzo yaliyokuwa yakiendelea. Kutoka kushoto ni Mkurugenzi Idara ya Mashariki ya Kati, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Hemedi Iddi Mgaza, Kamishna wa Petroli na Gesi Michael Mjinja, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Dkt. James Mataragio na Msaidizi wa Waziri, Wakili Dunford Mpelumbe.*

Mabalozi waliofanya mazungumzo na Makamba ni pamoja na Balozi Abdulaziz Hamad Alasim (Saudi Arabia), Balozi Hussain Ahmad Al-Homaid (Qatar), Balozi Khalifa Abdulrahman M.A Almarzooqi (UAE), na Balozi Ahmed Djellal (Algeria).

Baadhi ya viongozi waliohudhuria mazungumzo hayo ni pamoja na Kamishna wa Petroli na Gesi Michael Mjinja, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Joseph Edward Sokoine na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) Dkt. James Mataragio.



*Balozi wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) nchini Tanzania, Khalifa Abdulrahman M.A Almarzooqi akimwelezea jambo Waziri wa Nishati, January Makamba baada ya kukutana kwa mazungumzo, Oktoba 18, 2021 katika ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Nishati, January Makamba akimwelezea jambo Balozi wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) nchini Tanzania, Khalifa Abdulrahman M.A Almarzooqi baada ya kukutana kwa mazungumzo, Oktoba 18, 2021 katika ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dar es Salaam. Aliye pamoja nao (kushoto) ni Afisa Uhusiano wa Ubalozi, Saddam Ahmed Ali.*

# MAJADILIANO 'HGA' YANUKIA, WAZIRI MAKAMBA AKUTANA NA VIONGOZI EQUINOR



*Waziri wa Nishati January Makamba, (Wa pili kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Makamu wa Rais wa Equinor (Afrika) Paul McCafferty (kulia kwa waziri), Makamu wa Rais na Mwenyekiti Mkazi, Equinor Tanzania AS, Unni Merethe Skolstad Fjaer na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) Dkt. James Mataragio, mara baada ya kikao kifupi kilichofanyika Oktoba 21, 2021 katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati jijini Dar es Salaam.*

**Na Janeth Mesomapya**

Waziri wa Nishati January Makamba amekutana na kufanya mazungumzo na Makamu wa Rais wa kampuni ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia ya Equinor (Afrika) Paul McCafferty.

Viongozi hao walikutana Oktoba 21, 2021 katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Salaam. Mazungumzo hayo yalihudhuriwa pia na viongozi wengine wa Equinor na Shirika



*Makamu wa Rais wa Equinor (Afrika) Paul McCafferty akimweleza jambo Waziri wa Nishati January Makamba wakati wa kikao kifupi kilichofanyika Oktoba 21, 2021 katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati jijini Dar es Salaam. Pamoja nao, ni viongozi wengine wa Equinor na Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) waliohudhuria kikao hicho.*



*Waziri wa Nishati January Makamba akimsikiliza Makamu wa Rais wa Equinor (Afrika) Paul McCafferty wakati wa kikao kifupi kilichofanyika Oktoba 21, 2021 katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati jijini Dar es Salaam. Pamoja nao, ni viongozi wengine wa Equinor na Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) waliohudhuria kikao hicho.*

# MAJADILIANO 'HGA' YANUKIA, WAZIRI MAKAMBA AKUTANA NA VIONGOZI EQUINOR

la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC).

Imeelezwa kuwa mazungumzo hayo ni sehemu ya maandalizi ya majadiliano ya Mkataba wa Nchi Hodhi (HGA) wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (LNG) yanayotarajiwa kuanza rasmi Novemba 8, 2021.

Kwenye kikao hicho, McCafferty alimpongeza Waziri Makamba kwa niaba ya Serikali kwa hatua hiyo ya kuanza tena kwa majadiliano ya mkataba huo wa HGA kwani yatafungua njia kwaajili ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo wa LNG.

McCafferty alieleza kuwa Equinor iko tayari kwa majadiliano hayo na kuongeza kwamba mradi huo ni moja ya miradi yenye uwekezaji mkubwa inayotekelezwa na Equinor duniani, hivyo ni majadiliano muhimu katika kuweka msingi mzuri wa utekelezaji wake.

Equinor ni moja ya wabia wakuu wa utekelezaji wa mradi wa LNG ambao utasimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA). Wabia wengine ni pamoja na kampuni ya Shell na TPDC kwa niaba ya serikali.

Mradi wa LNG unakadiriwa kuwa wa thamani ya takriban Dola za Marekani bilioni 30 huku ukitarajiwa kutengeneza nafasi za ajira za moja kwa moja 6,000 na zisizo za moja kwa moja zaidi ya 15,000 kwa Watanzania.



*Waziri wa Nishati January Makamba akizungumza jambo na Makamu wa Rais wa Equinor (Afrika) Paul McCafferty wakati wa kikao kifupi kilichofanyika Oktoba 21, 2021 katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati jijini Dar es Salaam. Pamoja nao, ni Makamu wa Rais na Mwenyekiti Mkazi, Equinor Tanzania AS, Unni Merethe Skolstad Fjaer (katikati) na Mkuu wa Idara ya Mawasiliano Equinor Tanzania, Genevieve Kasanga.*

# Waziri wa Nishati afanya mazungumzo na Balozi wa Marekani na Uholanzi



*Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akizungumza na Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe De Boer katika Ofisi ndogo za Wizara ya Nishati mkoani Dar es Salaam tarehe 08 Oktoba, 2021. Mazungumzo yao yalihusu masuala mbalimbali kuhusu Sekta ya Nishati.*



*Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania, Wiebe De Boer (kushoto), akizungumza na Waziri wa Nishati, January Makamba katika Ofisi ndogo za Wizara ya Nishati mkoani Dar es Salaam tarehe 08 Oktoba, 2021. Mazungumzo ya viongozi hao yalihusu masuala mbalimbali kuhusu Sekta ya Nishati.*

Waziri wa Nishati, January Makamba amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Marekani nchini Tanzania Donald J.Wright pamoja na Balozi wa Uholanzi, Wiebe De Boer ambapo alitaja vipaumbele katika Sekta ya Nishati.

Mazungumzo yake na Mabalozi hao yalifanyika tarehe 8 Oktoba, 2021 katika Ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo mkoani Dar es Salaam na kuhudhuriwa na watendaji mbalimbali akiwemo Kamishna wa Umeme na Nishati na Jadidifu, Felchesmi Mramba, Kamishna wa Petroli na Gesi, Michael Mjinja, na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio.

Katika kikao chake na Balozi wa Marekani, Waziri Makamba alimueleza Balozi huyo vipaumbele mbalimbali vya Serikali katika Sekta ya Nishati ikiwemo upatikanaji wa umeme hasa katika maeneo ya vijijini, kwani Serikali imefanya kazi kubwa ya kupeleka umeme maeneo hayo lakini wananchi wengi bado wanahitaji huduma hiyo.

Alitaja kipaumbele kingine kuwa ni uwepo wa nishati endelevu za



*Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe De Boer mara baada ya kumaliza mazungumzo kuhusu Sekta ya Nishati nchini. Kikao kilifanyika katika Ofisi ndogo za Wizara ya Nishati mkoani Dar es Salaam tarehe 08 Oktoba, 2021.*



*Waziri wa Nishati, January Makamba (Wa Nne kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe De Boer (wa Nne kushoto) pamoja na viongozi kutoka Wizara ya Nishati na baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara mara baada ya kumalizika kwa kikao baina yao kilichofanyika katika Ofisi ndogo za Wizara ya Nishati mkoani Dar es Salaam tarehe 08 Oktoba, 2021.*

# Waziri wa Nishati afanya mazungumzo na Balozi wa Marekani na Uholanzi



*Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akizungumza na Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Donald J. Wright katika Ofisi ndogo za Wizara ya Nishati mkoani Dar es Salaam tarehe 08 Oktoba, 2021. Mazungumzo yao yalihusu masuala mbalimbali kuhusu Sekta ya Nishati.*

kupikia mfano gesi ya kwenye mitungi (LPG) ambayo itawafanya wananchi wengi waache kutumia mkaa na kuni kwa kupikia na hivyo kuondoa suala la uharibifu wa misitu ambalo pia linapelekea mabadiliko ya tabia nchi.

"Kipaumbele kingine, ni kuzifanya Taasisi zilizo chini ya Wizara kama vile TANESCO, TPDC na EWURA, kuwa na uwezo wa RasiliMali Watu pamoja na uwezo wa kifedha utakaoziwezesha Taasisi hizo kuwa na ufanisi pamoja na usimamizi madhubuti wa Sekta ya Nishati hasa katika kipindi ambacho Tanzania inaenda kuwa nchi yenye umeme wa kutosha katika ukanda huu." Alisema Makamba

Kwa upande wake Balozi wa Marekani, Donald J. Wright, alisema ataendelea kufanya kazi na Wizara na kwamba kumekuwa na ushirikiano wa takriban miaka 60 kati ya Tanzania na nchi hiyo na eneo mojawapo la ushirikiano huo ni sekta ya Nishati.

Katika mazungumzo yake na Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe De Boer, Waziri wa Nishati alitaja maeneo mbalimbali yanayohitaji ushirikiano, kubwa ikiwa ni kupeleka umeme katika maeneo ambayo hayajafikiwa na umeme wa gridi kama vile visiwa kwa kuweka mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali ikiwemo Jua ambalo linapatikana katika maeneo yote ya Tanzania.

Aliishukuru Uholanzi kwa kuwa na ushirikiano mzuri na Tanzania kwa miaka mingi na kwamba ushirikiano wa nchi hizo mbili upo katika sekta mbalimbali ikiwemo nishati.

Balozi wa Uholanzi, Wiebe De Boer alimweleza Waziri wa Nishati kuwa, Serikali isisite kuwasiliana na Ubalozi huo pale inapoona kuna uhitaji wa kuungwa mkono mkono katika utekelezaji wa mipango mbalimbali.



*Waziri wa Nishati, January Makamba (Wa Tatu kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Marekani nchini, Donald J.Wright (wa Nne kushoto) mara baada ya kumalizika kwa kikao kilichofanyika katika Ofisi ndogo za Wizara ya Nishati mkoani Dar es Salaam tarehe 08 Oktoba, 2021. Wengine katika picha ni Watendaji kutoka Wizara ya Nishati, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Ubalozi wa Marekani.*



*Afisa Biashara Mwandamizi katika Ubalozi wa Marekani, Ken Walsh (kushoto) akizungumza jambo wakati wa kikao cha Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) na Balozi wa Marekani nchini, Donald J.Wright kilichofanyika katika Ofisi ndogo za Wizara ya Nishati mkoani Dar es Salaam tarehe 08 Oktoba, 2021.*

# ALIYOZUNGUMZA NAIBU WAZIRI WA NISHATI, STEPHEN BYABATO KATIKA HAFLA YA MAKABIDHIANO YA LESENI YA UCHIMBAJI MKUBWA KWA KAMPUNI YA TEMBO NICKEL CORPORATION LTD NA UZINDUZI WA TAARIFA YA UHAMASISHAJI UWAZI NA UWAJIBIKAJI KATIKA SEKTA YA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA

>> Tutamfikishia mteja umeme ili aweze kufanya shughuli zake mara atakapokuwa tayari.

>> Nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuifanya Tanzania kuwa mjumbe wa TEITI inayowafanya wenye utajiri wa rasilimali madini, mafuta na gesi kushirikiana katika kuona mataifa yao yananufaika na uwepo wa rasilimali hizo.

>> Tanzania imeenda mbele zaidi ya kuandaa sheria mwaka 2015 yenye kanuni za mwaka 2019 na kufanyiwa marejeo mwaka 2021 yenye lengo la kusimamia tasnia muhimu ya uziduaji.

>> Sheria hiyo inayataka makampuni ya madini, mafuta na gesi kutoa taarifa ili kuiwezesha Serikali kujua umelipa kodi kiasi gani na umeyalipa kiasi gani makampuni binafsi yanayotoa huduma katika mgodi wako ili kuwa na uzani unaofanana

>> Faini ya kutokutoa taarifa hizo kwa makampuni yaliyowekeza kwenye tasnia ya uziduaji ni shilingi milioni 100 hii ni kuonesha kuwa serikali imedhamiria kuweka mazingira wezeshi yatakayowawezesha sekta binafsi na serikali kukaa pamoja na kujadiliana kuona mapato yanayotokana na rasilimali za mafuta, gesi na madini yanatumika katika uendelezaji wa eneo letu katika shughuli mbalimbali za maendeleo.

>> Wizara ya Nishati ni walengwa katika jambo hili, tunachimba gesi lakini pia Gesi Asilia kwa sasa inachangia asilimia 60 katika uzalishaji umeme na sasa tumejiandaa kuanza utekelezaji wa mradi wa LNG kutoka Lindi ambapo kiasi cha Dola za Marekani Bilioni 30 zitatumika kwenye mradi huo.

>> Wizara ya Nishati tupo tayari kutoa ushirikiano na kusimamia sheria kwani tunao



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato*

wajibu kwenye eneo hili.

>> Kutolewa kwa leseni ya uchimbaji mkubwa wa madini ni fusra kwa Wizara ya Nishati kwani tunapata mteja mpya kutokana na mahitaji ya umeme katika uendeshaji wa shughuli za mgodi.

>> Tuna taarifa kuwa mgodi utakapoanza utahitaji megawati 8, Mkoa wa Kagera kwa sasa unatumia takribani megawati 17 Serikali imejipanga kuhakikisha gridi ya Taifa inafika Mkoa wa Kagera mapema iwezekanavyo na kukamilisha mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi na mradi wa uzalishaji umeme wa Rusumo.

>> Tukikamilisha mradi wa Julius Nyerere, tukapata megawati 2115, tukakamilisha mradi wa Rusumo na kupata megawati 27 tutakuwa na umeme mwingi sana na hivyo niwahakikishie wawekezaji na wawekezaji wengine wanaotaka kuja kuwekeza Tanzania na tunaahidi kila atakayehitaji umeme atapata huduma hiyo.

# Waziri Makamba akutana na Waziri wa Nishati na Madini wa Algeria

**Algiers, Algeria**

Waziri wa Nishati, January Makamba tarehe 28 Oktoba 2021 amekutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Nishati na Madini wa Algeria, Mohamed Arkab.

Katika mazungumzo hayo, Waziri Makamba alieleza mahusiano ya kihistoria yaliyopo baina ya Tanzania na Algeria na kueleza nia ya Serikali ya Tanzania kuendeleza mahusiano hayo katika nyanja ya uchumi kwa mustakabali wa nchi hizi mbili .




*Waziri wa Nishati, January Makamba akifurahia jambo baada ya kukutana na Waziri wa Nishati na Madini wa Algeria, Mohamed Arkab, tarehe 28 Oktoba 2021.*

Akiongea katika kikao hicho, Waziri Makamba alisema "Tanzania na Algeria tumekuwa na mahusiano ambayo ni ya kihistoria na sasa Serikali ya Tanzania ingependa kuona mahusiano ya nchi zetu mbili yanaboreshwa zaidi kwa kuwa na mahusiano ya kiuchumi ambapo kwa kuanzia tunaangalia sekta ya nishati ambayo wenzetu Algeria mmepiga hatua kubwa".

Kwa upande wake, Waziri wa Nishati na Madini wa Algeria, Mohamed Arkab alieleza utayari uliopo ndani ya Serikali ya Algeria kushirikiana na Serikali ya Tanzania.

Waziri Arkab alisema "Kwanza tunafurahi sana kwa Serikali ya Tanzania kutaka kukuza mahusiano yetu zaidi na hususan katika eneo la kiuchumi ambalo ni kweli tuna nafasi ya kuboresha zaidi kwa manufaa ya nchi zetu mbili".

Waziri Arkab alifafanua zaidi kuwa, Algeria ina uzoefu mkubwa katika eneo la nishati ikijumuisha mafuta na gesi ambapo wanazalisha mafuta na gesi na kuuza ndani na nje ya Algeria na wateja wakubwa ni nchi za Ulaya kwa kuwa kijiografia wako karibu zaidi. "kupitia kampuni ya Taifa ya Mafuta, Sonatrach na kampuni



*Waziri wa Nishati, January Makamba akiwa katika kikao na Waziri wa Nishati na Madini wa Algeria, Mohamed Arkab. Wengine pichani upande wa kulia ni Mwambata wa Jeshi, Ubalozi wa Tanzania nchini Algeria, Brigedia Jenerali Adolf Peter Mutta, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio, Kamishna wa Petroli na Gesi, Ndg. Michael Mjinja, Balozi wa Tanzania nchini Algeria, Balozi Meja Jenerali Jacob Gideon Kingu, Katibu wa Waziri wa Nishati, Dunford Mpelumbe na Mwambata wa Siasa na Utamaduni Ubalozi wa Tanzania nchini Algeria, Suleiman Rashid.*

# Waziri Makamba akutana na Waziri wa Nishati na Madini wa Algeria

zake tanzu, tumeweza kujenga mtandao wa takribani kilometa 22,000 wa kusambaza gesi ndani ya nchi pamoja na bandari za kupakia mafuta katika maeneo mbalimbali ndani ya nchi" alisema Wazri Arkab.

katika ziara hiyo Waziri Makamba aliambatana na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio na Kamishna wa Petroli na Gesi, Michael Mjinja.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio alieleza fursa zilizopo katika mkondo wa juu na chini wa sekta ya mafuta na gesi nchini ambapo aliwakaribisha



*Waziri wa Nishati na Madini wa Algeria, Mohamed Arkab na timu yake wakisikiliza kwa makini mazungumzo ya timu ya Tanzania iliyoongozwa na Waziri wa Nishati, January Makamba*

Algeria kuwekeza na kushirikiana na TPDC katika maeneo hayo.

Tanzania imeingia katika uchumi wa kati ambapo mahitaji ya nishati ndani ya nchi yameongezeka na hivyo uwekezaji zaidi katika kusambaza gesi asilia ni muhimu na pia kuhakikisha tunaendelea kufanya shughuli za utafutaji ili kuendana na mahitaji yanayokuwa siku hadi siku, hivyo tunaamini ushirikiano baina ya nchi zetu ni muhimu kwa mustakabali wa nchi zetu" alieleza Dkt. Mataragio

Kwa upande wake Kamishna wa Petroli na Gesi, Ndg. Michael Mjinja alieleza uhitaji mkubwa wa nishati uliopo Tanzania na kusisitiza kuwa Algeria wanakaribishwa kwa mikono miwili kuwekeza nchini Tanzania.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Mkurugenzi Mkuu wa Sonatrach, Toufik Hakkar, Mkurugenzi Mkuu wa Sonelgaz, Chahar Boulakhras na maafisa waandamizi wengine kutoka Serikali ya Algeria pamoja na Balozi wa Tanzania nchini Algeria Balozi Meja Jenerali Jacob Gideon Kingu, Mwambata wa Jeshi, Brigedia Jenerali Adolf Peter Mutta na maafisa wengine kutoka Ubalozi wa Tanzania nchini Algeria.



*Waziri wa Nishati, January Makamba akiwa katika kikao na Waziri wa Nishati na Madini wa Algeria pamoja na Balozi wa Tanzania nchini Algeria, Balozi Meja Jenerali Jacob Gideon Kingu pamoja na timu ya Tanzania iliyoambatana na Waziri Makamba*

# Waziri Makamba afanya ziara ya kikazi nchini Saudi Arabia

**Riyadh, Saudi Arabia,**

Waziri wa Nishati, January Makamba amewasili nchini Saudi Arabia kwa ziara ya kikazi ya siku mbili kwa mualiko wa Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia, Abdulaziz bin Salman Al Saud.

Akiwa nchini humo Waziri Makamba anatarajiwa kushiriki hafla ya uzinduzi wa "Saudi Green Initiative" utakaofanyika Riyadh tarehe 23 Oktoba 2021 pamoja na kufanya mikutano ya kutangaza fursa za uwekezaji katika sekta ya Nishati nchini Tanzania.

Mapema baada ya kuwasilia nchini humo, Waziri Makamba alikutana na kufanya mazungumzo na Mhandisi Faisal Ali Al Swayed kutoka kampuni ya Advanced Electronics Company na Mhandisi Adil Saleh Alomair, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati Jadidifu (Renewable Energy).



*Waziri wa Nishati, January Makamba (wa pili kulia) akiwa katika mazungumzo na Mhadisi Adil Saleh Alomair, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati Jadidifu (wa kwanza kushoto) na Mhandisi Faisal Ali Al Swayed kutoka kampuni ya Advanced Electronics Company (wa pili kushoto) katika Makazi ya Balozi wa Tanzania nchini Saudia Arabia. Wa kwanza kulia ni Balozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia, Ally J. Mwadini.*

Akizungumza na Mha. Faisal Ali Al Swayed, Waziri Makamba alisema "Tanzania imepiga hatua kubwa katika usambazaji wa nishati za gesi asilia na umeme lakini bado kuna uhitaji wa vifaa kama vile mita za kisasa za Gesi Asilia na Umeme kuendana na kasi ya usambazaji na teknolojia kwa ujumla".

Aidha, Waziri Makamba alieleza nia ya Serikali kutumia zaidi teknolojia kukomesha tatizo la wizi na upotevu wa nishati jambo ambalo linarudisha nyuma juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kuwapatia wananchi nishati ya uhakika.

"Moja ya kazi kubwa tuliyonayo sasa ni kuangalia namna tunaweza kutumia teknolojia kukomesha changamoto hii" alieleza Waziri Makamba na kuwakaribisha wataalamu hao kutembelea Tanzania kwa lengo la kuangalia fursa mbalimbali za uwekezaji katika sekta ya Nishati.

Kwa upande wake Mha. Faisal alimhakikishia Waziri Makamba kuwa kampuni yake ina uwezo mkubwa wa kuzalisha mita kwa kuzingatia mahitaji ya mteja na kuahidi kuendelea kuwasiliana na Ubalozi kwa lengo la kuwekeza nchini Tanzania.

Katika ziara hiyo, Waziri wa Nishati, January Makamba aliambatana na Kamishna wa Petroli na Gesi, Michael Mjinja na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio.



*Waziri wa Nishati, January Makamba akiwa katika mazungumzo na Mhandisi Faisal Ali Al Swayed kutoka kampuni ya Advanced Electronics Company (kushoto) huku Balozi wa Tanzania nchini Saudia Arabia Balozi Ally J. Mwadini (kushoto kwa Waziri), Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio (wa kwanza kulia), Kamishna wa Petroli na Gesi, Michael Mjinja (wa pili kulia) wakifuatilia kwa makini mazungumzo hayo.*

# Waziri Makamba aanza kutekeleza agizo la Makamu wa Rais mkoani Kigoma

**Na Teresia Mhagama, Kigoma**

Waziri wa Nishati, January Makamba ameanza kutekeleza agizo lililotolewa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt.Philip Mpango tarehe 22 Septemba 2021 la kutatua changamoto ya kukatika umeme mara kwa mara mkoani Kigoma.

Katika ziara yake ya kikazi mkoani Kigoma aliyoifanya tarehe 06 Oktoba 2021, Waziri Makamba alibainisha kuwa, kuna mipango ya muda mfupi, kati na mrefu ambayo inalenga kuhakikisha kuwa Mkoa wa Kigoma unakuwa na umeme wa uhakika na hivyo kuondoa kero hiyo ya umeme kukatika mara kwa mara.



*Waziri wa Nishati, January Makamba akiwa katika chumba cha kuongozea mitambo ya umeme katika Kituo cha kuzalisha umeme kilichopo Kigoma mjini tarehe 06 Oktoba, 2021. Kushoto kwa Waziri ni Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Ester Mahawe.*

Alibainisha kuwa, katika mipango ya muda mfupi, Kituo cha umeme cha Kigoma chenye uwezo wa megawati 6.25 kitaongezewa mashine mbili zitakazozalisha jumla ya megawati 2.5 kwenye kituo husika ambapo mashine ya kwanza yenye uwezo wa megawati 1.25 itakamilika kufungwa tarehe 15 Novemba 2021.

Aliongeza kuwa, mashine ya pili yenye uwezo wa megawati 1.25 itafungwa na kukamilika tarehe 25 Novemba 2021.

Aidha, alieleza kuwa miradi ya muda wa kati na mrefu itaunganisha Kigoma na umeme wa gridi na kupelekea Mkoa huo kuwa na umeme mwingi na wa bei nafuu kwani kwa sasa Kigoma inatumia umeme unaotokana na mafuta na hivyo inatumia shilingi Bilioni 3 kwa mwezi kuzalisha nishati hiyo huku mapato



*Waziri wa Nishati, January Makamba (Wa Tatu kutoka kulia) akitazama moja ya mitambo ya kuzalisha umeme katika Kituo cha kuzalisha umeme kilichopo wilayani Kasulu mkoa wa Kigoma tarehe 06 Oktoba, 2021. Kushoto kwa Waziri ni Naibu Mkurugenzi Mtendaji (Uzalishaji) kutoka TANESCO, Mhandisi Pakaya Mtamakaya.*



*Waziri wa Nishati, January Makamba (Wa Tatu kutoka kulia) akiwa katika kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia Jua wilayani Kigoma Mkoa wa Kigoma kinachomilikiwa na kampuni ya Nextgen Solawazi. Kulia kwa Waziri ni Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Ester Mahawe. Wengine katika picha ni Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande (wa kwanza Kushoto), na Wa Pili kutoka kushoto ni Naibu Mkurugenzi Mtendaji (Uzalishaji) kutoka TANESCO, Mhandisi Pakaya Mtamakaya.*

# Waziri Makamba aanza kutekeleza agizo la Makamu wa Rais mkoani Kigoma

yakiwa ni shilingi bilioni 1.5.

Miradi hiyo ya muda wa kati na mrefu itakayounganisha Kigoma na gridi ya Taifa ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme itakayotoka Nyakanazi-Kakonko hadi Kibondo itakayokamilika Machi 2022

Mradi mwingine ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Kigoma ambayo inatarajiwa kukamilika Oktoba 2022.

Aidha, mradi mwingine ni ujenzi wa njia kubwa ya umeme ya msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma ambapo utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kukamilika mwaka 2023

Vilevile mradi mwingine wa umeme unaotarajiwa kuboresha hali ya umeme mkoani Kigoma ni mradi wa kufua umeme wa maji wa Malagarasi utakaozalisha megawati 49.5 na Serikali imeshapata fedha kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) na mwakani atatafutwa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi.

Akiwa mkoani Kigoma, Waziri Makamba alikagua mitambo ya kuzalisha umeme iliyopo wilayani Kigoma na Kasulu ambapo akiwa wilayani Kasulu alikuta changamoto ya mitaa mingi kukosa umeme ambapo ili kutatua changamoto hiyo alieleza kwamba utafanyika utaratibu ndani ya Wizara ili kuiwezesha TANESCO kupeleka umeme kwenye mitaa hiyo.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Nishati alitembelea kituo cha umeme wa Jua cha Nextgen Solawazi ambacho kwa sasa kinazalisha umeme wa kiasi cha megawati 1.8 na kupeleka kwenye kituo cha kuzalisha umeme cha TANESCO.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa TANESCO, Maharage Chande, alisema kuwa, Mkoa wa Kigoma utaanza kupata umeme wa gridi ya Taifa ifikapo Machi 2022.

Katika ziara hiyo Waziri wa Nishati aliambatana na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Kigoma wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Kigoma Ester Mahawe ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Kigoma.



*Waziri wa Nishati, January Makamba (Wa Pili kushoto) akitazama baadhi ya mitambo ya umeme katika Kituo cha kuzalisha umeme kilichopo wilayani Kasulu mkoa wa Kigoma tarehe 06 Oktoba, 2021. Kushoto kwa Waziri ni Naibu Mkurugenzi Mtendaji (Uzalishaji) kutoka TANESCO, Mhandisi Pakaya Mtamakaya na kulia kwa Waziri ni Mkuu wa Kituo cha umeme cha Kasulu, Masanja Nkuba.*



*Waziri wa Nishati, January Makamba akizungumza na Wataalam kutoka TANESCO wanaofanya kazi katika Kituo cha kuzalisha umeme kilichopo wilayani Kasulu mkoani Kigoma wakati alipofika mkoani humo kutatua changamoto ya upatikanaji umeme wa uhakika.*

**Hafsa Omar-Dodoma**

# TAASISI YA UTAFITI YATAKIWA KUISHIRIKISHA SERIKALI

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali ameitaka Taasisi inayojishughulisha na utafiti ya (Natural Resource Governance Institute) kuishirikisha Serikali kwenye tafiti zinazohusu Serikali ili kuwa na usahihi wa takwimu zinazotolewa.

Ameyasema hayo, Oktoba 29,2021 wakati wa kikao cha Wizara ya Nishati na Taasisi hiyo kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Nishati, zilizopo katika mji wa Serikali, jijini Dodoma ambapo Taasisi hiyo iliwasilisha tafiti yao



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali akizungumza wakati wa kikao cha Wizara ya Nishati na Taasisi ya Natural Resource Governance Institute, kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Nishati, zilizopo katika mji wa Serikali, jijini Dodoma. Oktoba 29,2021.*



*Mkurugenzi wa Sera Mipango, Petro Lyatuu (kwanza-kulia) Kamishna Msaidizi wa Nishati Jadidifu, Edward Ishegoma (katikati) Kamishna Msaidizi wa Gesi, Mohamed Fakihi (kwanza-kushoto) wakimsikiza muwasilishaji wa utafiti wa kuhusiana na rasilimali ya Gesi Asilia nchini Tanzania, Silas Okin'g (hayupo pichani),katika kikao cha kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Nishati, zilizopo katika mji wa Serikali, jijini Dodoma. Oktoba 29,2021.*



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (katikati) akiendesha kikao cha Wizara ya Nishati na Taasisi ya Natural Resource Governance Institute, kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Nishati, zilizopo katika mji wa Serikali, jijini Dodoma. Oktoba 29,2021.*

# TAASISI YA UTAFITI YATAKIWA KUISHIRIKISHA SERIKALI

kuhusiana na rasilimali ya Gesi Asilia nchini Tanzania.

Aidha, alisema ushirikiano wa Serikali na Taasisi hizo utasaidia kupata takwimu zilizo sahihi ambazo zitakuwa zenye manufaa kwa Taifa kiujumla.

"Haipendeza tafiti mbalimbali kusambazwa kwa wananchi bila ya Serikali kushirikishwa na kutoa maoni yao unapofanya tafiti lazima ungalie na upande wa pili ambao ni Serikali," alisisitiza Mahimbali.

Alisema, Serikali itaendelea kufanya kazi na kushirikiana na Taasisi hiyo katika tafiti mbalimbali na kwakuwa inaisadia Serikali kupata takwimu mbalimbali muhimu.

Kikao hicho, kilihudhiriwa na Kamishna Msaidizi wa Gesi, Mohamed Fakihi, Kamishna Msaidizi wa Nishati Jadidifu, Edward Ishegoma, Mkurugenzi wa Sera Mipango Petro Lyatuu pamoja na watumishi mbalimbali wa Wizara ya Nishati na Taasisi zilizopo chini yake.







*Picha mbalimbali za matukio kwenye kikao cha Wizara ya Nishati na Taasisi ya Natural Resource Governance Institute kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Nishati, zilizopo katika mji wa Serikali, jijini Dodoma*

# WAZIRI MAKAMBA AWASILISHA UJUMBE MAALUM WA RAIS SAMIA KWA RAIS WA UMOJA WA FALME ZA KIARABU

**Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu**

Waziri wa Nishati, January Makamba, amewasilisha Ujumbe Maalum wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda kwa Mhe. Khalifa Bin Zayed Al Nahyan, Rais wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Waziri Makamba aliwasilisha ujumbe huo maalum kupitia kwa Sheikh Shakhbout bin Nahyan Al Nahyan, Waziri wa Nchi anayeshughulikia mambo ya nje, tarehe 24 Oktoba, 2021 katika Ofisi za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ya UAE.



*Waziri wa Nishati, January Makamba (kushoto) akiwasilisha ujumbe maalum Maalum wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda kwa Mhe. Khalifa Bin Zayed Al Nahyan, Rais wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).Anayepokea ni Sheikh Shakhbout bin Nahyan Al Nahyan, Waziri wa Nchi anayeshughulikia mambo ya nje UAE.*

Mheshimiwa Makamba yupo Umoja wa Falme za Kiarabu kwa ziara ya kikazi kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika masuala ya Mafuta na Gesi

Mheshimiwa Makamba katika mazungumzo hayo ameambatana na Mhe. Mohamed Mtonga, Balozi wa Tanzania katika Umoja wa Falme za Kiarabu, Kamishina wa Petroli na Gesi, Michael Mjinja kutoka Wizara ya Nishati pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio.



*Waziri wa Nishati, January Makamba (kushoto) akizungumza na Sheikh Shakhbout bin Nahyan Al Nahyan, Waziri wa Nchi anayeshughulikia mambo ya nje katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) wakati Waziri Makamba alipofika nchini humo akiwa na ujumbe Maalum wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda kwa Mhe. Khalifa Bin Zayed Al Nahyan, Rais wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).*

# Waziri Makamba akutana na ADNOC

**Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu**



*Waziri wa Nishati, January Makamba (wa nne kutoka kulia) akiwa katika mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa ADNOC Global Trading Ltd, Ahmed Bin Thalith. Wengine pichani wanaofuatilia mazungumzo hayo ni Balozi wa Tanzania UAE, Balozi Mohamed Mtonga (wa tatu kutoka kulia), Kamishna wa Petroli na Gesi kutoka Wizara ya Nishati Tanzania, Michael Mjinja (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio (wa kwanza kulia)*

Waziri wa Nishati, January Makamba amekutana na kufanya mazungumzo na Kampuni ya Mafuta ya Taifa ya Abu Dhabi (ADNOC). Waziri Makamba amefanya kikao hicho tarehe 25 Oktoba 2021 na Mkurugenzi Mkuu wa ADNOC Global Trading Ltd, Ndg. Ahmed Bin Thalith ambapo walijadili masuala mbalimbali ikiwemo kudumisha uhusiano baina ya Tanzania na Abu Dhabi katika sekta ya mafuta na gesi.

Waziri Makamba pia alipata nafasi ya kutembelea ofisi za ADNOC na kujionea matumizi ya hali ya juu ya teknolojia katika kuendesha na kusimamia biashara ya mafuta.

"Tanzania tuna nafasi kubwa ya kujifunza kutoka kwa wenzetu kama Abu Dhabi ambao wamekuwepo katika sekta ya mafuta na gesi kwa muda mrefu na ziara hii ni sehemu ya kujifunza huko" alisema Waziri Makamba.

Waziri Makamba aliambatana na Balozi wa Tanzania nchini UAE Balozi Mohamed Mtonga, Kamishna wa Petroli na Gesi kutoka Wizara ya Nishati Tanzania, Michael Mjinja na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio.



*Waziri wa Nishati, January Makamba (wa kwanza kulia) akizungumza jambo na Mkurugenzi Mkuu wa ADNOC Global Trading Ltd, Ahmed Bin Thalith wakati wa kutembelea ofisi za ADNOC kujionea namna wanavyoendesha na kusimamia biashara ya mafuta. Wengine pichani ni Kamishna wa Petroli na Mafuta, Michael Mjinja (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio (wa tatu kulia)*



*Waziri wa Nishati, January Makamba na ujumbe aliombatana nao wakisindikizwa na wenyeji wao baada ya kufanya kikao na ziara katika ofisi za ADNOC, Abu Dhabi.*

# WATALAAM KUTOKA BARA NA ZANZIBAR WAKUTANA

**Hafsa Omar-Dodoma**



*Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Nishati, Petro Lyatuu ( mbele-kushoto), Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asili Zanzibar (ZPDC), Mikidadi Rashidi(mbele-kulia) wakiendesha kikao cha Ushirikiano baina ya Wizara hizo kilichofanyika Oktoba 27,mwaka huu katika ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo katika Mji wa Serikali jijini Dodoma*

Wataalam kutoka Wizara ya Nishati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na wa kutoka katika Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wamefanya kikao cha Ushirikiano kwa ngazi ya wataalam.

Kikao hicho cha Ushirikiano baina ya Wizara hizo kimefanyika Oktoba 27, mwaka huu katika ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo katika Mji wa Serikali jijini Dodoma.

Kikao hicho, kimeongozwa na Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Nishati, Petro Lyatuu na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asili Zanzibar (ZPDC), Mikidadi Rashidi na kuhudhiriwa na Wajumbe kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zake pamoja na wajumbe kutoka katika Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na Taasisi zilizopo chini yake.

Wajumbe wa kikao, walijadili ajenda mbalimbali ambazo ni hatua zilizofikiwa katika kukamilisha hati



*Washiriki kutoka Wizara ya Nishati Pamoja na Taasisi zilizopo chini yake wakiwa katika kikao cha Ushirikiano baina ya Wizara ya Nishati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kilichofanyika Oktoba 27, mwaka huu katika ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo katika Mji wa Serikali jijini Dodoma.*



*Washiriki Kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na Taasisi zilizopo chini yake wakiwa katika kikao cha Ushirikiano baina ya Wizara ya Nishati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kilichofanyika Oktoba 27, mwaka huu katika ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo katika Mji wa Serikali jijini Dodoma.*

# WATALAAM KUTOKA BARA NA ZANZIBAR WAKUTANA

ya Mashirikiano(MoU) kati ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) na Mamlaka ya Udhibiti Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta Asilia, Zanzibar (ZPRA), hatua iliyofikiwa katika kukamilisha hati ya mashirikiano (MoU) kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asili Zanzibar (ZPDC) na masuala mengine mbalimbali.

Wakati akifungua kikao, Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Nishati, Petro Lyatuu, aliwataka wajumbe hao kutoa michango yao kwa ufanisi.

Kikao hicho ni moja ya vikao ambavyo vinafanyika kwa kuzingatia muongozo uliotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais, ambavyo hupaswa kufanyika mara nne kwa mwaka.







*Picha mbalimbali za matukio katika kikao na baada ya kikao cha Ushirikiano baina ya Wizara ya Nishati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kilichofanyika Oktoba 27, mwaka huu katika ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo katika Mji wa Serikali jijini Dodoma.*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA NISHATI**

**TAARIFA KWA UMMA**

**Taarifa ya ziara ya Waziri wa Nishati katika nchi zinazozalisha mafuta na gesi**

***Arusha,***
***Jumapili, 31 Oktoba 2021***

Kama inavyofahamika, bei ya mafuta ghafi duniani imeendelea kupanda kwa kasi na kwa kiwango kikubwa, kutoka dola 50 kwa pipa mwezi wa Januari mwaka huu hadi dola 86 kwa pipa leo tarehe 31 Oktoba 2021. Hali hii inapelekea bei kupanda kwenye vituo vya kuuzia mafuta na mitaani hapa nchini.

Kama itakavyokumbukwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, alielekeza hatua mbalimbali za kikodi, kisheria/kanuni na kiutawala ili kupunguza makali na athari za ongezeko hili la bei. Wizara ya Nishati imeanza kutekeleza maelekezo hayo na pia kuratibu hatua mbalimbali za Wizara na taasisi nyingine za umma na kufanikiwa kupunguza ongezeko kubwa la bei ya mafuta kwa mwezi wa Oktoba.

Katika kutimiza azma ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba bei za mafuta haziumizi wananchi, na shughuli za uchumi haziathiriki, Wizara ya Nishati ilichunguza na kubaini uwezekano wa unafuu wa bei iwapo Serikali yenyewe itanunua mafuta moja kwa moja kutoka kwenye mitambo ya kusafisha mafuta (refineries) ya nchi rafiki badala ya kuachia watu wa katikati (intermediaries) kununua kwa nchi hizo hizo rafiki zetu na kutuuzia kwa bei kubwa.

Kutokana na hilo, katika duru la kwanza, kuanzia tarehe 22 hadi 29 Oktoba 2021 nilifanya ziara katika nchi tatu – Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu na Algeria – ambazo zinazalisha mafuta kwa wingi na kuuza kote duniani. Katika nchi hizo, nilikutana na Mawaziri wenzangu wa Nishati, na viongozi wengine waandamizi wa Serikali na makampuni

# Nishati na Hazina hakuna mbabe SHIMIWI hatua ya Makundi




*Wachezaji wa Timu ya Mpira wa Pete Wanawake Wizara ya Nishati wakifunga goli dhidi ya Sanaa katika Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara, Taasisi na Idara za Serikali (SHIMIWI) kwa hatua za Makundi, iliyochezwa katika uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro, Oktoba 22, 2021.*

**Na Zuena Msuya, Morogoro**

Timu ya Mpira wa Miguu ya Wizara ya Nishati imetoka sare ya kutokufungana na Timu ya Hazina, mpira uliochezwa kwa dakika 60 uwanjani katika mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara, Taasisi na Idara za Serikali (SHIMIWI) kwa hatua za Makundi.

Mchezo huo umechezwa katika Uwanja wa Jamhuri Mkoani Morogoro Oktoba 22, 2021 ikiwa ni mchezo wa kwanza kwa Timu ya Nishati na mchezo wa pili kwa Timu ya Hazina.

Kwa mujibu wa Nahodha wa timu ya Nishati, Fadhil Msigwa wachezaji wote wako salama kuendelea na mashindani hayo akieleza kuwa (kesho) Oktoba 23, 2021, timu hiyo itacheza na Wakala wa Taifa wa Kuhifadhi Chakula(NFRA)

Kwa upande wa Mpira wa Pete, Timu ya Nishati imecheza Dakika 40 uwanjani dhidi ya Sanaa,Wizara ya Nishati imepata Magoli 21 dhidi ya mpinzani wake iliyepata magoli 23 katika mashindano hayo.

Nahodha wa Nishati, Fortunata Getele ameeleza kuwa timu yake imefanya vizuri sana lakini imeshindwa kutoka na ushindi kutokana kwakuwa na wachezaji majeruhi wengi.

Kesho Oktoba 23, 2021 timu ya mpira wa pete itacheza na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Timu zote mbili ni Hazina na Sanaa wamecheza michezo miwili katika hatua za makundi.



*Wachezaji wa Timu ya Mpira Wanaume, Wizara ya Nishati waliocheza katika mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara, Taasisi na Idara za Serikali (SHIMIWI) kwa hatua za Makundi, iliyochezwa katika uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro, Oktoba 22, 2021.*

# Nishati yaibuka kidedea hatua ya makundi SHIMIWI




*Wachezaji wa Timu ya Mpira wa Pete wa Wizara ya Nishati (wenye sare ya bluu) wakisubiria mpira waliorusha golini, katika Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Taasisi na Idara za Serikali (SHIMIWI) katika hatua za Makundi dhidi ya Tume ya Walimu, Oktoba 21, 2021 katika uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro.*

**Na Zuena Msuya**
**Morogoro**

Timu ya Mpira wa Pete ya Wizara ya Nishati imeiubuka mshindi dhidi ya Tume ya Walimu kwa kuwafunga magoli 14 kwa 5, katika Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Taasisi na Idara za Serikali (SHIMIWI) katika hatua za Makundi.

Mchezo huo ulichezwa dakika 40 katika Uwanja wa Jamhuri Mkoani Morogoro, Oktoba 21, 2021, ambapo kipindi cha kwanza kwa ya mapumziko Nishati waliongoza kwa magoli Tisa wakati Tume ya Walimu wakiwa na magoli 3.

Akizungumzia mchezo huo, Nahodha wa Timu ya Nishati, Fortunata Getele alieleza kuwa kipindi cha pili cha mchezo huo Nishati ilijiongezea ushindi zaidi kwa kuongeza magoli mengine 5, na Tume ya Walimu magoli 2, na kuipa ushindi Nishati kwa Magoli 14 dhidi ya Tume ya Walimu iliyoambulia magoli 5 tu katika kipindi chote cha mchezo.

Katika hatua za makundi katika mashindano ya SHIMIWI, Wizara ya Nishati imepangwa katika kundi "A" ikicheza na Timu ya Wizara ya Sanaa, Tamaduni na Michezo, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi(OSHA), Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, pamoja na Tume ya Walimu.

Michezo hiyo bado inaendelea hadi Novemba 2, 2021.




*Wachezaji wa timu ya mpira wa Pete wa Wizara ya Nishati wakiwa tayari kwa Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Taasisi na Idara za Serikali (SHIMIWI) katika hatua za Makundi dhidi ya Tume ya Walimu, Oktoba 21, 2021 katika uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro.*




*Wachezaji wa timu ya mpira wa Pete wa Wizara ya Nishati ( wenye sare ya Bluu) wakicheza katika Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Taasisi na Idara za Serikali (SHIMIWI) katika hatua za Makundi dhidi ya Tume ya Walimu, Oktoba 21, 2021 katika uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro.*

# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI




*www.nishati.go.tz*

*Wizara ya Nishati*

*@Nishati2017*

*wizara_ya_nishati_tanzania*

*Wizara ya Nishati*

***Fika Ofisi ya Mawasiliano,***
**Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au**
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi** +255-26-2320148